# JARIDA LA USHIRIKA

ISSN 2714-2175, Toleo Na: 014 Julai - Septemba, 2023.




## TUNAMUUNGANISHA MKULIMA NA MNUNUZI KUPITIA VYAMA VYA USHIRIKA ILI KUMPATIA BEI NZURI - *Rais Dkt. Samia*







*"Ushirika - Pamoja Tujenge Uchumi Imara na Endelevu"*

# KUTOKA KWA MRAJIS

## MCHANGO WA VYAMA VYA USHIRIKA KATIKA KUKUZA UCHUMI



**Dkt. Benson Ndiege,**
Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji
Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC)

Ndugu Msomaji,

Tume kupitia Ushirika imefanikiwa kuboresha maisha ya wananchi kupitia shughuli wanazozifanya zinazowaingizia kipato kwa muunganiko wa Ushirika. Kwa mfano, wakulima wameweza kulipwa fedha zao za mazao kwa uharaka baada ya kuuza mazao yao kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala. Tume imeendelea kufanya Usimamizi thabiti wa Vyama vya Ushirika ambao umechangia kwa kiasi kikubwa katika ongezeko la Pato la Taifa. Mfano, kati ya mwaka 2019/2020 hadi 2021/2022 jumla ya Tani 9,804,347 za mazao ya kimkakati ziliuzwa kupitia Vyama vya Ushirika, na jumla ya Shilingi 2,917,816,152,983.61 zililipwa kwa wakulima.

Vilevile, Serikali inakusanya tozo na kodi mbalimbali kupitia Mamlaka zake zikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia Vyama vya ushirika. Mfano, Serikali katika mwaka 2021/2022 ilipokea jumla ya Shilingi 15,144,077,319.16 zikiwa ni fedha za ushuru unaotokana na zao la korosho uliolipwa na vyama vya TANECU, MAMCU, RUNALI, LINDI MWAMBAO, TAMCU na CORECU. Vilevile, jumla ya Shilingi 1,041,957,051.00 zimepokelewa kama ushuru kutoka katika Vyama vya Ushirika vya KDCU na KCU kupitia zao la kahawa.

Viwanda Vidogo, vya Kati na Vikubwa 279 vimeanzishwa nchini kupitia Mfumo wa Uendeshaji wa Vyama vya Ushirika. Katika Msimu wa 2022/2023 Vyama Vya Ushirika vilitumia jumla ya Shillingi 397,706,245,786 kununua pembejeo za kilimo kwa ajili ya wakulima wa zao la Korosho, Kahawa, Tumbaku na Pamba. Tume pia kupitia Vyama vya Ushirika imeendelea kuratibu masoko na biashara ya zao la Ufuta nchini ambapo katika msimu wa 2022/2023 jumla ya kilo 79,170,426 zenye thamani ya Shilingi 245,130,400,328.00 zimeuzwa kupitia ushirika katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Pwani na Songwe na kuwezesha Halmashauri zake kupata ushuru wa zao wenye thamani ya Shilling 6,022,450,313.00

Tume vilevile inasimamia Vyama vya Ushirika vya Kifedha (SACCOS) ambapo hadi kufikia mwaka 2021 kabla ya kuanza kutekeleza Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha kulikuwa na SACCOS 3,831 zenye thamani ya Shilingi Trilioni 1.6 na Akiba ya Shilingi Bilioni 803 pamoja na Amana za Shilingi Bilioni 149.2. Baada ya usajili mpya kwa mujibu wa Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha, hadi kufikia mwezi Novemba, 2022 kuna jumla ya SACCOS 743 zenye wanachama 1,731,237 wenye Amana za Shilingi Bilioni 713.6, Mali za Shilingi Bilioni 945.3 na Hisa zenye thamani ya Shilingi Bilioni 149.2.

Kutokana na mafanikio yanayopatikana, Vyama vya Ushirika chini ya usimamizi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika vinafanya kazi nzuri ya kukuza kipato na uchumi wa wananchi. Kwa hiyo, Watanzania walioko katika sekta zote wanaendelea kuhimizwa kujiunga katika Vyama vya Ushirika ili waweze kuinua uchumi wao na wa Taifa kwa ujumla.

Endelea kupata elimu, habari na matukio mbalimbali ya Ushirika kupitia Jarida hili.

Karibu sana

# MHE. RAIS DKT. SAMIA SULUHU HASSAN ATEMBELEA ‘KIJIJI CHA USHIRIKA’ NDANI YA NANENANE




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akimsikiliza Dkt. Benson Ndiege, Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) alipotembelea katika mabanda ya ‘Kijiji cha Ushirika’ kwenye Maonesho ya Wakulima (nanenane) jijini Mbeya tarehe 08 Agosti, 2023*

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan tarehe 08 Agosti, 2023 alitembelea ‘Kijiji cha Ushirika’ na kujionea shughuli mbalimbali zinazofanywa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Wadau na Wanaushirika kwa ujumla katika Maonesho ya Kwanza ya Kimataifa ya Wakulima katika Viwanja vya John Mwakangale Jijini Mbeya.

Akiwa katika Kijiji cha Ushirika, Dkt. Samia alielezwa na Mrajis wa Vyama Vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege kuhusu kazi mbalimbali zinazofanywa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika na wadau wa Ushirika katika kuimarisha maendeleo ya Ushirika nchini.

Akizungumza na Wakulima, Wanaushirika na Wananchi kwa ujumla katika Kilele cha Maonesho hayo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliitaka Benki ya Maendeleo ya Kilimo nchini (TADB) kuiongezea nguvu Benki ya Ushirika Kilimanjaro (KCBL) ili kuweza kuwasaidia Wanaushirika kuwa na benki yao (Benki ya Taifa ya Ushirika) na kuwawezesha kupata mikopo kwa riba nafuu.

"Wakati nazunguka mabandani, niliingia katika ‘kijiji cha Ushirika’, wameniambia mikopo kupitia mabenki inawapa usumbufu kidogo kwa maana hiyo wanaanzisha benki yao, sasa TADB jikung'uteni kidogo muunge juhudi za Washirika ili Ile Benki yao iweze kusimama vizuri," alisema Mhe. Rais

# RAIS DKT. SAMIA AKABIDHI TREKTA KWA ISOWELU AMCOS




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akimkabidhi funguo za Trekta Mwenyekiti wa ISOWELU AMCOS Bw. Chesco Ng'eve katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya kimataifa ya Wakulima Duniani yaliyofanyika katika viwanja vya John Mwakangale Jijini Mbeya*

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, amekabidhi zawadi ya Trekta kwa Chama cha Msingi cha Ushirika cha ISOWELU AMCOS kilichopo mkoani Njombe ikiwa ni kutambua juhudi za uzalishaji wa mazao kwa kiwango kikubwa zaidi kwa mwaka 2022. Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amekabidhi trekta hilo tarehe 08 Agosti, 2023 kwa Mwenyekiti wa Chama hicho, Chesco Ng'eve, wakati wa Kilele cha Maadhimisho ya Kwanza ya Kimataifa ya Wakulima yaliyofanyika kitaifa katika viwanja vya John Mwakangale Jijini Mbeya. Akizungumza mara baada ya kupokea Trekta hilo Mwenyekiti wa ISOWELU AMCOS Bw. Ng'eve alisema kuwa amefarijika sana kupokea zawadi hiyo kutoka kwa Rais kwani itakwenda kusaidia kukuza uchumi wa wanachama na AMCOS kukua zaidi.

"Zawadi ina staha zake, nimejisikia vizuri sana kupokea zawadi kutoka kwa Serikali, zawadi ambayo itakwenda kukuza uchumi wa Chama, nimejisikia furaha sana sana tena mno, kitendo cha kutangazwa kwamba ISOWELU AMCOS wanapata Trekta na mpokeaji ni Mwenyekiti Chesco Ng'eve, ilikuwa ni furaha mno sio kidogo," alisema Mwenyekiti. Aidha, Mwenyekiti ameishukuru Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania kwa kuwa mstari wa mbele kuwashauri na kuwapa mafunzo, hasa ya MUVU ambayo yamewasaidia sana kufikia hatua hiyo. *"Naipongeza sana Tume ya Maendeleo ya Ushirika, lakini sisahau kuwashukuru wakulima kuelewa yale sisi tunayaona na kuwaelekeza wao kama viongozi kisha kuyapokea na kuyafanyia kazi," alisema Chesco.*

# TUNAMUUNGANISHA MKULIMA NA MNUNUZI KUPITIA VYAMA VYA USHIRIKA ILI KUMPATIA BEI NZURI - RAIS DKT. SAMIA




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza wakati wa kikao cha Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF) kilichofanyika Jijini Dar es salaam Septemba 7, 2023*

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, alisema Serikali imeamua kumuunganisha mkulima na mnunuzi pamoja kupitia Vyama vya Ushirika vya wakulima kwa lengo la kuwawezesha wanunuzi kushindana kwenye minada na hivyo kupandisha bei za mazao ya Mkulima.

"Tumeshuhudia mara kadhaa bei ya Korosho ikipanda kwasababu kuna Ushirika wa Mkulima, na mnunuaji moja kwa moja, hivyo tumewaondoa watu wa kati ambao walikuwa wanakwenda moja kwa moja kununua mazao shambani na wananunua kwa bei ndogo," alisema Mhe. Rais Samia.

Mhe. Dkt. Samia ameyasema hayo Septemba 7, 2023 katika Mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF) wakati akijibu maswali kutoka Kwa wadau kwenye mkutano uliohusisha vijana, ambapo ametumia nafasi hiyo kuelezea hatua ambazo Serikali inazichukua kuondoa changamoto ya soko kwa wakulima.

“Tumeshuhudia hivi karibuni zao la Ufuta kwasababu tumeingiza kwenye Ushirika na tumetumia Mfumo wa Stakabadhi Ghalani, wakulima wanapeleka mazao yao huko kwenye Ushirika, wanunuaji wanashindanishwa bei inapanda,” alisema Mhe. Rais Samia.

Mhe. Rais Samia amesema katika zao la Mbaazi ambalo miaka miwili, mitatu nyuma wakulima walihamasishwa walime sana na wakalima lakini kwasababu Wakulima hawakuunganishwa na soko na hawakuwa na mipango mizuri Mbaazi zilianguka bei sana na kuwavunja moyo wakulima.

“Mwaka jana (2022) mbaazi iliuzwa kwa Sh.300 kwa kilo lakini mwaka huu (2023) wakulima wameuza kwa zaidi ya Shilingi 2,000 kwa kilo. Sasa huu ndio mtindo tutakaokwenda nao kwenye mazao mengine pia ili kumuunganisha mkulima na soko,” alisema Mhe. Rais.

# LINDI KUJENGWA KIWANDA CHA KUBANGUA KOROSHO



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt.Samia Suluhu Hassan akizungumza na Wananchi wakati wa mkutano wa hadhara uliofanyika Mitwero Lindi Mjini Septemba 15, 2023.*

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alisema katika mkoa wa Lindi kutajengwa kiwanda kimoja cha kubangua Korosho, ili ifikapo mwaka 2025 Korosho zote kutoka Tanzania zitauzwa zikiwa zimebanguliwa.

Alisema hayo Septemba 19, 2023 wakati wa Mkutano wa hadhara wa mwisho uliofanyika Mitwero Lindi Mjini ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya kikazi iliyoanzia Mkoani Mtwara Septemba 15, 2023.

Mheshimiwa Rais alisema kiwanda hicho kikiazishwa kitatoa ajira kwa wananchi wa Lindi na kitaongeza thamani ya Korosho sokoni ambayo itamfanya mkulima kuzidi kunufaika kutokana na mauzo ya Korosho zake.

“Niwatake wakulima mzidishe juhudi katika uzalishaji ili ikifika kipindi cha kuuza Korosho iliyobanguliwe tuwe na Korosho ghafi za kutosha kuingiza kiwandani, “alisema Mhe. Rais Samia.

# WAKULIMA JIUNGENI KWENYE VYAMA VYA USHIRIKA - MAKAMU WA RAIS



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdori Mipango akihutubia wakati akifungua Maadhimisho ya Maonesho ya kwanza ya Kimataifa ya Wakulima, Wafugaji na Wavuvi yaliyofanyika katika viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya Agosti 01, 2023*

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango alitoa rai kwa Wakulima kujiunga na Vyama vya Ushirika ili kupata nguvu ya pamoja ya soko la mazao yao na kuwa na chanzo cha Mikopo na kuimarisha Maendeleo ya Ushirika hapa nchini.

"Kwa kutambua umuhimu wa Ushirika katika kuwaweka wakulima pamoja, Serikali inaendelea kuwahamasisha Wakulima, Wafugaji na Wavuvi kujiunga kwenye Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo yaani SACCOS vitakavyokuwa chanzo cha mikopo kwaajili ya kuendeleza shughuli zao na kuimarisha uwekezaji, katika Kilimo na Uvuvi lakini pia viwanda vya kusindika mazao ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi," alisema Makamu wa Rais

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango alitoa rai kwa Wakulima kujiunga na Vyama vya Ushirika ili kupata nguvu ya pamoja ya soko la mazao yao na kuwa na chanzo cha Mikopo na kuimarisha Maendeleo ya Ushirika hapa nchini. "Kwa kutambua umuhimu wa Ushirika katika kuwaweka wakulima pamoja, Serikali inaendelea kuwahamasisha Wakulima, Wafugaji na Wavuvi kujiunga kwenye Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo yaani SACCOS vitakavyokuwa chanzo cha mikopo kwaajili ya kuendeleza shughuli zao na kuimarisha uwekezaji, katika Kilimo na Uvuvi lakini pia viwanda vya kusindika mazao ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi," alisema Makamu wa Rais.

Makamu wa Rais alitoa rai hiyo wakati akifungua Maadhimisho ya Maonesho ya Kwanza ya Kimataifa ya Wakulima alimaarufu Nanenane yaliyofanyika tarehe 01 Agost hadi tarehe 8 Agosti, 2023 katika Viwanja vya John Mwakangale Jijini Mbeya yenye kauli mbiu: ***"Vijana na Wanawake ni Msingi Imara wa Mifumo endelevu ya Chakula".***

# MAFANIKIO YA SEKTA YA USHIRIKA KWA MWAKA 2022/2023 NA

# MPANGOWA KUIMARISHA USHIRIKA KWA MWAKA 2023/2024

## 1. UTANGULIZI

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) ni Idara inayojitegemea chini ya Wizara ya Kilimo iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013. Majukumu ya Tume ni Udhibiti na Usimamizi wa Vyama pamoja na Uhamasishaji wa Maendeleo ya Ushirika nchini. Sekta ndogo ya Ushirika ni Sekta wezeshi inayojumuisha Vyama vya Ushirika vya aina mbalimbali vilivyoko katika Sekta za Kilimo, Fedha, Madini, Mifugo, Viwanda na Usafirishaji.

## 2. UTEKELEZAJI KATIKA MWAKA 2022/ 2023

Tume kwa mwaka wa Fedha 2022/23 imefanya kazi katika misingi ya Kusimamia na Kuhamasisha Ushirika kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya Mwaka 2013 pamoja na kuweka vipaumbele vya utekelezaji kwa mwaka 2023/2024 katika maeneo ya Uwekezaji katika mifumo ya kisasa ya kidijitali, uanzishwaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika, Kuhamasisha mfumo wa Ushirika kujiendesha kibiashara, Kuboresha Sera, Sheria na usimamizi wa Ushirika, Kuhamasisha Ushirika kwenye sekta mbalimbali na makundi maalum, na Kuimarisha uwekezaji wa mali za Ushirika katika uzalishaji. .

### 2.1 USIMAMIZI NA UDHIBITI WA VYAMA VYA USHIRIKA

Katika kutekeleza jukumu la Usimamizi na Udhibiti wa Vyama vya Ushirika, Tume imetekeleza kazi zifuatazo:

#### 2.1.1 Usajili wa Vyama vya Ushirika na Wanachama

Tume ya Maendeleo ya Ushirika hadi kufikia mwezi Juni 2023, imesajili jumla ya Vyama vya Ushirika **7,300;** kati ya hivyo, **77** ni Vyama vya Upili, **1** ni Shirikisho la Vyama vya Ushirika, **4,252** ni Vyama vya Ushirika wa Kilimo na Masoko (AMCOS), **2,034** ni Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) na **936** ni Vyama vinavyojishughulisha na kazi mbalimbali zikiwemo, ufugaji na uvuvi.

Aidha, idadi ya wanachama wa Vyama vya Ushirika imeongezeka kutoka wanachama **6,965,272** mwaka 2021/2022 hadi **8,358,326** kufikia mwaka 2022/2023. Ongezeko hilo limetokana na uhamasishaji kuhusu umuhimu wa wananchi kujiunga na Ushirika ili kuwawezesha kupata nguvu ya pamoja ya soko na mitaji.

#### 2.1.2 Usimamizi wa Vyama vya Kifedha

Tume imekasimishwa na Benki Kuu ya Tanzania (BOT) Mamlaka ya kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Na.10 ya Mwaka 2018 pamoja na Kanuni zake za Mwaka 2019. Katika kutekeleza jukumu hilo, hadi kufikia Juni 2023 Tume imepokea maombi ya Leseni za SACCOS **1,183** na kufanya tathmini ambapo jumla ya SACCOS **789** zilikidhi vigezo vya matakwa ya Sheria ya Huduma Ndogo ya Fedha pamoja na Kanuni zake na kupewa Leseni za uendeshaji wa biashara ya Huduma Ndogo za Fedha hapa nchini.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, mikopo iliyotolewa na SACCOS kwa wanachama wake iliongezeka kutoka Shilingi 1,500,943,078,699 (Shilingi 1.5 Trilioni) hadi Shilingi 1,680,101,297,056 (Shilingi 1.7 Trilioni). Akiba za wanachama wa SACCOS ziliongezeka kufikia Shilingi 790,911,090,750 (Shilingi 790.9 Bilioni) kutoka Shilingi 740,777,390, 907 (Shilingi 740.8 Bilioni) kwa mwaka uliopita.

Aidha, Akiba na Amana za SACCOS ziliongezeka kwa asilimia 7.8 kutoka Shilingi 793.87 Bilioni mwaka 2021/2022 hadi kufikia Shilingi 855.91 Bilioni mwaka 2022/2023. Ongezeko la Akiba na Amana lilizisaidia SACCOS kutoa mikopo zaidi kwa wanachama wake ukilinganisha na mwaka uliopita. Hisa za SACCOS ziliongezeka kutoka Shilingi 184.74 Bilioni mwaka 2021/2022 hadi kufikia Shilingi 205.85 Bilioni mwaka 2022/2023, ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 11.4.

#### 2.1.3 Ukaguzi kwenye Vyama vya Ushirika

Tume hufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika Vyama vya Ushirika. Lengo la kaguzi hizo ni kubaini uzingatiwaji wa matakwa ya Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali inayohusiana na utendaji wa Vyama vya Ushirika.

Katika kipindi cha mwaka 2022/2023 hadi kufikia Juni, 2023 TCDC ilifanya ukaguzi wa jumla ya Vyama vya Ushirika **4,712** kati ya vyama **7,300** vya ushirika kupitia Ofisi ya Tume Makao Makuu na Ofisi za Warajis Wasaidizi wa Mikoa.

i. **Masuala yaliyobainika:**

Matokeo ya kaguzi hizo yalionesha kuwepo kwa mapungufu katika utendaji wa Vyama vya Ushirika hususan maeneo ya uandishi wa vitabu, urasimishaji wa mali za Vyama, utunzaji wa nyaraka na kumbukumbu nyingine za Vyama, uzingatiaji wa miongozo ya Mrajis, na madeni ya muda mrefu katika taasisi za kifedha.

ii. **Hatua zilizochukuliwa:**

Hatua zilizochukuliwa kwa Vyama vya Ushirika ni kuvunja Bodi **55** za Vyama vya Ushirika, kupeleka masuala **30** Polisi na masuala **47** yanashughulikiwa na TAKUKURU. Aidha, viongozi wa vyama waliobainika kukiuka sheria na Kanuni za vyama vya ushirika walitakiwa kujieleza; na Tume imetoa mafunzo kwa watendaji 4,732 wa Vyama vya Ushirika kuhusu uandishi wa vitabu.

iii. **Jitihada za kukabiliana na masuala yaliyobainika:**

Jitihada zinazotekelezwa na Tume kwa kushirikiana na Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO), Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) na wadau wengine ni kama zifuatazo:-

a) **Mpango Maalum wa Mafunzo kwa Maafisa Ushirika na watendaji wa Vyama**

Hadi kufikia Juni, 2023 Maafisa Ushirika kutoka mikoa 16 ya Tanzania Bara walipatiwa mafunzo ya Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama. Mikoa hiyo ni Mtwara, Lindi, Ruvuma, Njombe, Iringa, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Kagera, Mara, Kigoma, Simiyu na Geita, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam.

b) **Mpango wa Mafunzo kwa Viongozi na Watendaji wa Vyama**

Tume kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Ushiriki (TFC), Chama Kikuu cha Ushirika na Mikopo (SCCULT), Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) na Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) imetoa Mafunzo kuhusu uandishi wa vitabu, uendeshaji na usimamizi wa Vyama vya Ushirika ngazi ya chama, Sheria ya Ushirika, utatuzi wa migogoro na uwekezaji yalitolewa kwa viongozi na watendaji 23,953 wa vyama. Tume pia, ilitoa Mafunzo kuhusu matumizi ya Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU) kwa Maafisa ushirika 222 na Watendaji wa Vyama 4,732 na Watendaji wa Bodi 74 za Mazao. Mafunzo hayo ni katika kutekeleza Mpango wa Mafunzo kwa Viongozi na Watendaji wa Vyama mwaka 2022/2023 ulioandaliwa na kutekelezwa na TFC, SCCULT, MoCU, COASCO na TFC.

### c) Kuboresha mazingira ya Kazi

Tume imeendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa Maafisa Ushirika kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa vyama vya ushirika. Katika mwaka 2022/2023 hadi kufikia mwezi Machi 2023, Tume ilinunua kompyuta 226, viti 70, magari 12 na pikipiki 147. Aidha, Tume imepokea magari matatu (3) kutoka Wizara ya Fedha na gari moja (1) kutoka Taasisi isiyo ya kiserikali (Heifer International) kwa ajili ya Ofisi za mikoa. Hadi kufikia mwaka 2022/2023, Warajis Wasaidizi wa mikoa 20 wamepatiwa magari, na ni Mikoa 6 tu bado haijapatiwa magari.

### *d)* Kuandaa na kuanza Matumizi ya Mfumo wa kidigitali wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU)

Tume kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) imetenngeneza Mfumo wa Kidigitali wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU), unaolenga kurahisisha usimamizi na uendeshaji wa Vyama vya Ushirika kwa nia ya kuongeza ufanisi, uwazi na uwajibikaji. Sambamba na kuboresha utendaji, mfumo huu unasaidia kupunguza gharama za uendeshaji, kuwa na uhakika wa kupata takwimu na kuimarisha utendaji/uendeshaji wa Vyama. Hadi kufikia Juni 2023, vyama vya Ushirika 5,424 kati 7,300 vimesajiliwa katika Mfumo wa kidigitali wa MUVU.

### e) Kufanya Ufuatiliaji wa matumizi ya Miongozo ya Usimamizi wa Vyama vya Ushirika

Tume ya Maendeleo ya Ushirika imefanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miongozo 15 ya Usimamizi wa Vyama vya Ushirika inayolenga kuongeza elimu, uwazi na uadilifu katika uendeshaji wa shughuli za Vyama nchini. Aidha, Tume inafanya ufuatiliaji wa namna vyama vya ushirika vinavyozingatia miongozo hiyo katika utendaji wake wa kila siku.

### f) Kuimarisha Huduma za Kisheria kwa Vyama

Ili kuimarisha Utendaji wa vyama vya Ushirika, Tume inatekeleza Mpango wa Mafunzo kwa Watekelezaji wa Sheria (Law enforcers) 62 kutoka Mikoa ya Tanzania Bara. Lengo la mafunzo ni kupanua wigo wa utoaji huduma za kisheria katika Vyama vya Ushirika kwa ngazi ya Mikoa na Wilaya, ili kupunguza migogoro kwenye Vyama na kuondoa dosari katika utendaji wa vyama vya ushirika.

## 2.2 UHAMASISHAJI

Katika kutekeleza jukumu la Uhamisishaji, Tume ya Maendeleo ya Ushirika imetekeleza kazi zifuatazo:

### 2.2.1 Uhamasishaji wa Uanzishwaji wa Vyama vya ushirika vya Mbogamboga

Tume ya Maendeleo ya Ushirika imefanya Uhamasishaji wa Uanzishwaji wa Vyama vya Ushirika vya Mbogamboga katika Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Iringa, Njombe, Mbeya na Songwe ambapo jumla ya wananchi 8,807 wakiwa kwenye vikundi 222 wamefikiwa na kuelimishwa juu ya Ushirika na manufaa ya kuanzisha Vyama vya Ushirika vya mbogamboga, ambapo Vyama 18 vimesajiliwa.

### 2.2.2 Kuandaa na kufanikisha Majukwaa ya Ushirika ya Mikoa

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 Mikoa 24 kati ya 26 ilifanya Majukwaa ya Ushirika ya Mikoa. Majukwaa haya yanalenga kukutanisha wadau wa Sekta ya Ushirika katika ngazi ya Mkoa ili kutafuta ufumbuzi wa changamoto mbalimbali zilizopo kwenye Mkoa husika. Aidha, changamoto zilizo nje ya uwezo wa Kimkoa huwasilishwa katika kongamano kuu la Siku ya Ushirika Duniani kwa lengo la kujadiliwa na kupatiwa suluhu.

### 2.2.3 Uingizwaji wa Mitaala ya Elimu ya Ushirika katika Masomo ya Elimu ya Msingi, Sekondari na Uanzishwaji wa Klabu za Ushirika Mashuleni.

Tume kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi zinazosimamia uendeshaji wa Elimu nchini zinafanyia kazi uwezekano wa kuingiza Elimu ya Ushirika katika Mitaala ya Elimu ya Msingi na Sekondari. Aidha, kwa sasa Tume imeandaa Mwongozo wa kuanzishwa kwa *Klabu za Ushirika* katika Shule za Sekondari na Msingi.

### 2.2.4 Miradi ya Ufugaji na Uendelezaji wa Maziwa

Tume ya Maendeleo ya Ushirika inashirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Taasisi ya *Heifer International* katika maeneo ya ukuzaji wa ufugaji na uendelezaji wa sekta ya maziwa chini ya Mradi wa *East Africa Dairy Development II* na *Tanzania Milk Processing Project.* Ambapo wananchi wamepatiwa miundombinu ya ufugaji na uendelezaji wa sekta ya maziwa yenye thamani ya **Shilingi 522,607,290.00.** Mradi umeanza kutekelezwa pia kwa Kanda ya Ziwa na inatarajiwa kuwa kupitia Mradi huu vyama vya ushirika vya ufugaji 88 vitaanzishwa.

### 2.2.5 Uanzishwaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika (KCBL)

Tume ya Maendeleo ya Ushirika katika mwaka 2022/2023 imeendelea kuhamasisha uanzishwaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika ili kutatua changamoto ya mtaji katika uendeshaji wa vyama vya ushirika nchini. Mikakati mbalimbali inatekelezwa itakayowezesha upatikanaji wa mtaji wa **Shilingi Bilioni 15** unaotakiwa kisheria ili iweze kusajiliwa kama Benki ya Taifa ya Ushirika. Uhamasishaji uliofanyika, umewezesha Mtaji wa Benki ya KCBL kuongezeka kutoka **Shilingi Bilioni 1.7** mwaka 2020/2021 hadi kufikia **Shilingi Bilioni 5.2** Mei, 2023.

### 2.2.6 Uendelezaji wa Viwanda kwenye Vyama vya Ushirika

Tume inaendelea kuhamasisha na kuratibu uanzishwaji wa viwanda kupitia Vyama vya Ushirika. Katika mwaka 2022/2023, viwanda viwili (2) vimeanza kujengwa yaani Kiwanda cha kubangua korosho kinachojengwa na TANECU Ltd kilichopo Newala Mkoani Mtwara na Kiwanda cha Vifungashio kinachojengwa na SONAMCU Ltd kilichopo mkoani Ruvuma. Kiwanda cha kubangua korosho kitakuwa na uwezo wa kubangua tani 3,500 za korosho kwa mwaka na kinatarajia kutoa ajira 500 kwa wananchi. Kiwanda cha kuchakata Pamba mkoani Simiyu cha Chama Kikuu cha Ushirika SIMCU (Sola) kimekarabatiwa na kinafanya kazi, huku kiwanda cha kuchakata Kahawa cha Chama Kikuu cha WAMACU Mkoani Mara kinajengwa na mashine zimeanza kusimikwa.

### 2.2.7 Kuimarisha biashara ya mazao ya wakulima

#### 2.2.7.1 Taarifa ya Mauzo ya Mazao yaliyouzwa kupitia Ushirika

Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa kushirikiana na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala, Bodi za Mazao Nchini Soko la Bidhaa Tanzania, Sekretarieti za Mikoa, Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji, Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na wadau wengine, katika mwaka 2022/2023 imeendelea kuratibu na kusimamia uendeshwaji wa minada, masoko na mauzo ya mazao ya wakulima kupitia Vyama vya Ushirika Nchini.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023, jumla ya **kilo 1,826,850,970** (sawa na tani **1,826,850.97**) zenye thamani ya **shilingi 1,752,128,795,530** (Shilingi **1.75 Trilioni**) ziliuzwa kutoka kwenye mazao ya tumbaku, korosho, pamba, kahawa, ufuta, kakao, mkonge, chai, mbaazi, soya, zabibu, miwa na maharage.

#### 2.2.7.2 Taarifa ya Malipo kwa wakulima

Kufuatia mauzo ya mazao yaliyofanyika, malipo halisi waliyopokea wakulima baada ya makato yalifikia jumla ya Shillingi **1,560,131,402,133 (**Shillingi **1.56 Trilioni)** kwa **kilo 1,826,850,971 (1.83 Bilioni)** zilizouzwa.

Mfano, Malipo kwa wakulima wa Ufuta Shilingi 237,940,321,511 **(**Shillingi **237.94 Bilioni)**, Korosho 301,480,167,362 **(**Shillingi **301.48 Bilioni),** Pamba Shilingi 313,256,754,000 **(**Shillingi **313.23 Bilioni )**, Kahawa Shilingi 357,755,593,782 **(**Shillingi **357.76 Bilioni),** Tumbaku Shilingi 125,356,612,017 **( Shillingi 125.36** Bilioni**)**, Kakao Shilingi 37,534,104,708 **(**Shillingi **37.53 Bilioni)**, Mkonge Shilingi 9,256,190,425 **(**Shillingi **9.26 Bilioni)**, na Chai Shilingi 87,384,878,573 (Shillingi **87.38 Bilioni**).

**2.2.7.3 Hali ya upatikanaji na usambazaji wa pembejeo**

Katika kuhakikisha kuwa wakulima na wanachama wa Vyama vya Ushirika wanahudumiwa kwa kusogezewa huduma karibu, Vyama vya ushirika vimekuwa vikiratibu upatikanaji pamoja na usambazaji wa pembejeo za kilimo. Hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2023, jumla ya shilingi 449,922,623,196 (Shilingi 449.92 Bilioni) zilitumika kunununua pembejeo za kilimo kupitia Vyama vya Ushirika nchini kwa ajili ya wakulima kwa mazao mbalimbali.

Mbolea iliyonunuliwa na kusambazwa kwa wakulima kupitia vyama vya ushirika ni Tani 1,266,435 yenye thamani ya 227,983,187,800 (Shillingi 227.98 Bilioni).

**2.8 Upatikanaji wa huduma za ugani kupitia Vyama vya Ushirika**

Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeendelea kuhamasisha Vyama vya Ushirika kuhusu umuhimu wa upatinakaji wa huduma za ugani na pembejeo kwa wanachama kwa wakati. Hadi sasa, Vyama vikuu vya Ushirika vimeajiri maafisa ugani 175 ambao wameendeleea kutoa huduma za ugani kwa wakulima katika mazao ya Tumbaku, Korosho, Pamba na Kahawa.

**2.9 Kuongeza uelewa wa Umma kuhusu Ushirika Katika kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano,**

Tume imetekeleza programu za kuhabarisha umma na wadau kuhusu mafanikio ya maendeleo ya Ushirika kupitia vipindi na makala zilizoandaliwa na kutangazwa kwenye Televisheni, Redio, Magazeti na Mitandao ya kijamii.

Katika mwaka 2022/2023 vipindi na makala 35 za TV ziliandaliwa na kutangazwa kupitia vituo vya Televisheni vya TBC1 na ITV. Aidha, Tume iliandaa na kutangaza vipindi 15 vya Redio. Tume imeandaa, kuchapa na kusambaza matoleo manne (4) ya Jarida la Ushirika.

## 3.0 MWELEKEO WA TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA KATIKA KUIMARISHA USHIRIKA KWA MWAKA 2023/2024

Utendaji wa kila siku wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika umelenga kwenye Kuimarisha Maendeleo ya Ushirika. Hivyo, Tume ya Maendeleo ya Ushirika ambayo inahusisha Kamisheni, Menejimenti na Watumishi wengine, imejipanga katika mwaka 2023/2024 kutekeleza maeneo saba (7) ya Kimkakati yatakayolenga kufikia Kipaumbele hicho. Maeneo hayo ni:

i) Uwekezaji katika mifumo ya kisasa ya kidijitali ili kuongeza ufanisi wa kiutendaji katika Vyama vya Ushirika, pamoja na Mamlaka za Usimamizi;

ii) Kuharakisha mchakato wa uanzishwaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika ili kuviwezesha Vyama vya Ushirika kupata Mikopo yenye Riba nafuu;

iii) Kuhamasisha mfumo wa Ushirika kujiendesha kibiashara wenye kuaminika na shindani ukijikita kwenye kuongeza thamani ya uzalishaji katika Vyama;

iv) Kuboresha Sera, Sheria na usimamizi wa Ushirika ili kuchochea ukuaji na maendeleo ya Ushirika imara Tanzania;

v) Kuhamasisha Ushirika kwenye sekta mbalimbali na makundi maalum ili kuhakikisha wananchi wengi zaidi wananufaika na mfumo wa Ushirika;

vi) Kuimarisha uwekezaji wa mali za Ushirika katika uzalishaji; na

vii) Kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutatua changamoto zilizopo kwenye Ushirika.

# USHIRIKA KUENDESHWA KIDIGITALI - MRAJIS




*Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Dkt .Benson Ndiege akiongea na Vyombo vya Habari kwenye ukumbi wa Habari Maelezo tarehe 11 Agosti,2023*

Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege, amesema Tume itaendelea kusimamia Vyama vya Ushirika kwa kutumia njia za kisasa za Kidigitali ambazo zinaongeza tija, ufanisi, uwazi na uwajibikaji na utakaosaidia kuimarisha na kuendeleza Ushirika nchini. Akiongea wakati wa kikao na Waandishi wa Habari kwenye Ofisi za Idara ya Habari - MAELEZO Agosti 11, 2023 Jijini Dodoma alisema hadi kufikia Juni 2023, vyama vya Ushirika 5,424 kati 7,300 vimesajiliwa katika Mfumo wa kidigitali wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU).

“Mfumo wa MUVU unasaidia kupunguza gharama za uendeshaji, kuwa na uhakika wa kupata takwimu na kuimarisha utendaji/uendeshaji wa Vyama,” alisema Mrajis Ameongeza kuwa kupitia Mfumo wa MUVU, Vyama vya Ushirika vinaweza kuwasilisha taarifa za Ukaguzi, mapato na matumizi ya Vyama, taarifa ambazo zinawasilishwa kwa urahisi na kuwafikia Maafisa Ushirika wa Wilaya, Warajis wasaidizi wa Mikoa na Ofisi ya Mrajis Taifa kwa lengo la kusimamia utendaji wa Vyama pamoja na kupunguza gharama za uendeshaji.

Aidha, Tume katika jitihada za kuimarisha Ushirika Mrajis alisema kuwa mwaka 2022/2023 imeendelea kuhamasisha uanzishwaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika (KCBL) ili kutatua changamoto ya mtaji katika uendeshaji wa vyama vya ushirika nchini. Mikakati mbalimbali inatekelezwa itakayowezesha upatikanaji wa mtaji wa Shilingi Bilioni 15 unaotakiwa kisheria ili iweze kusajiliwa kama Benki ya Taifa ya Ushirika.

Pamoja na mambo mengine Mrajis alisema vipaumbele vya Tume ni pamoja na kuhamasisha mfumo wa Ushirika kujiendesha kibiashara, kuhamasisha Ushirika kwenye sekta mbalimbali na makundi maalum ili kuhakikisha wananchi wengi zaidi wananufaika na mfumo wa Ushirika.

Aidha, Mrajis alisema TCDC imedhamiria kuimarisha uwekezaji wa mali za Ushirika katika uzalishaji; na kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutatua changamoto zilizopo kwenye Ushirika.

# SERIKALI KUONGEZA NGUVU YA USHIRIKA KUJIENDESHA KIBIASHARA




*Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Bashe akizungumza kwenye kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani yaliyofanyika katika viwanja vya Ipuli Nanenane Mjini Tabora.*

Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe, amesema Serikali itaendelea kuimarisha Ushirika kwa kuongeza tija katika Kilimo kitakachochangia kuinua uzalishaji wa mazao na kuongeza nguvu ya Ushirika kujiendesha kibiashara.

Mhe. Bashe ameyasema hayo wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani Julai 01, 2023 katika Viwanja vya Nanenane Ipuli Mjini Tabora yaliyofanyika Mkoani humo kuanzia Juni 26, 2023.

Akiongea na Wanaushirika alisema Serikali inafanya kazi kubadilisha kilimo cha Wakulima nchini ili kiweze kuwa chenye uzalishaji mkubwa wa mazao kwa kuongeza na kuimarisha miundombinu ya Kilimo hususani kilimo cha umwagiliaji hadi kufikia kiasi cha Hekari Millioni 8 ifikapo 2030. Hivyo, kuongeza uzalishaji wa mazao yatakayouzwa kupitia Ushirika utakaonufaisha wakulima kibiashara.

Aidha, Waziri wa Kilimo alisema Serikali itaendelea kuwekeza fedha na kurasimisha Kilimo ili wakulima nchini waweze kutumia mifumo inayotambulika rasmi na kuwapa urahisi wa kufanya biashara. Akieleza baadhi ya jitihada hizo ni pamoja na kuongeza miradi zaidi ya kilimo, kuendelea kutoa ruzuku za pembejeo, vitendea kazi ambavyo muelekeo wa Serikali ni kutekeleza kupitia Vyama vya Ushirika.

Mhe. Bashe amewataka wafanyabiashara kununua mazao ya wakulima kwa vipimo sahihi ili wakulima waweze kupata malipo sahihi yanayoendana na uzalishaji wa mazao yao. Akipongeza matumizi ya mizani ya kidijitali pamoja na Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU), mizani hizo tayari zimeanza kutumika katika mazao ya Kahawa Mkoani Kagera na Ufuta mkoani Lindi na kutoa rai mizani hizo kuendelea kutumika katika mazao mengine.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Abdulmajid Nsekela, alisema miongoni mwa vipaumbele vya Tume katika kuimarisha na kuongeza tija ya Ushirika, Kamisheni itaendelea kusimamia mchakato wa uanzishwaji wa Benki ya Taifa ya Biashara (KCBL). Amebainisha kuwa kupitia Benki hii Vyama vya Ushirika vitanufaika na huduma mbalimbali ikiwemo upatikanaji wa mikopo, Benki hiyo itamilikiwa na Wanaushirika kwa asilimia 51 na Sekta binafsi asilimia 49.

Amesema Tume itaendelea kuvijengea uwezo vyama ili vijiendeshe kibiashara kwa kuzingatia masuala ya utoaji huduma bora, ubunifu na kujitangaza. Pamoja na mambo mengine alisema Tume itasimamia Vyama vya Ushirika kuimarisha Uwekezaji wa mali za Ushirika katika Uzalishaji ikiwemo mashamba, maghala na ujenzi wa viwanda.

Ameongeza kuwa Tume itaendelea na jitihada za kuhamasisha Ushirika kwenye Sekta mbalimbali na makundi maalum ili kuhakikisha kuwa wananchi wengi zaidi wananufaika na Mfumo wa Ushirika. Ameongeza kuwa Vyama vya Ushirika 18 vya mazao ya bustani vimesajiliwa na uhamasishaji unaendelea pia katika Sekta ya Madini na nyingine unaendelea.

Maadhimisho hayo yamefanyika Mkoani Tabora kwa mara ya tatu yakiwa na kauli mbiu "Ushirika kwa Maendeleo Endelevu" yakihusisha Maonesho, makongamano, michezo, kujali jamii na majadiliano mbalimbali ya kuimarisha na kuendeleza Ushirika.

# VYAMA VYA USHIRIKA VYATAKIWA KUNUSA FURSA ZA KIBIASHARA




*Mrajis Msaidizi Masoko na Uwekezaji Revocatus Nyagilo akitoa maelezo kwa Mrajis wa vyama vya Ushirika Dkt. Benson Ndiege katika Maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara yaliyofanyika Jijini Dar es salaam*

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege amevitaka Vyama vya Ushirika kushiriki Maonesho ya Kimataifa ya Biashara, makongamano na ziara za kibiashara kwa lengo la kujifunza, kufanya biashara na kuongeza wigo wa uzalishaji ili kukimbizana na fursa zilizopo na zinazojitokeza.

"Zama hizi wanaushirika wanatakiwa kutambua Ushirika ni biashara hivyo wachangamke katika kufanya Ushirika wa kibiashara na kuufanya Ushirika kuwa ni kimbilio la kila Mtanzania," alisema Dkt. Ndiege.

Alitoa kauli hiyo tarehe 09/07/2023 alipotembelea mabanda ya Ushirika katika Maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara maarufu SABASABA kwenye viwanja vya Mwl Julius Kambarage Nyerere.

Mrajis alisema maonesho hayo ni sehemu ya fursa kwa vyama vya ushirika na wanapaswa kutumia fursa hiyo ili waweze kuongeza fursa za kibiashara ndani na nje ya Vyama vyao. Aidha, Dkt. Ndiege amevielekeza vyama vinavyofanya shughuli zaidi ya moja kuacha kuanziasha Vyama vingine isipokuwa waanze kuhuisha Masharti yao na kukifanya chama chao kuwa ni chama cha Ushirika wa Mazao mchanganyiko.

Naye Meneja wa Chama cha Ushirika cha DASICO LTD, Sijaona Mageta, alisema kupitia Sabasaba wamepata Kujitangaza na wanaendelea kupata oda kutoka kwa watu mbalimbali wanaohitaji huduma za thamani za majumbani na ofisini.

# VYAMA VYA USHIRIKA KATIKA MAONESHO YA SABASABA 2023




*Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika (Masoko na Uwekezaji) Revocatus Nyagilo pamoja na Afisa Ushirika Ndimwolo Laizer walipotembelea mabanda ya Ushirika katika Maonesho ya Kimataifa ya Biashara (sababsaba) yaliyofanyika Jijini Dar es salaam.*

Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika (Masoko na Uwekezaji), Revocatus Nyagilo alitembelea Mabanda ya Vyama vya Ushirika katika Maonesho ya 47 ya Kimataifa ya Biashara maarufu Sabasaba Julai 07, 2023 kwenye viwanja vya Mwl. Julius Kambarage Nyerere Jijini Dar es salaam.

Alitoa rai kwa Vyama vya Ushirika kuchangamkia fursa za kimasoko zinazopatikana kutoka mataifa mbalimbali na kuhakikisha wanachakata mazao yanayozalishwa ili kupata bidhaa zitakazokidhi ushindani wa soko huria.

Aidha, ameshauri Vyama kuajiri wataalam wenye uzoefu wa kutafuta masoko ya mazao na bidhaa za Vyama pamoja na kutafuta taarifa za masoko na kufahamu washindani katika soko la ushindani.

Vilevile alisema Viongozi wa Vyama waache kufanya kazi kwa mazoea bali kwa kufuata misingi, taratibu na Sheria ya Vyama vya Ushirika. Pia, viongozi wa Vyama vya Ushirika kuhakikisha wanachama wao hawauzi Mazao yao kwa mfumo usio rasmi kwani huchangia uchumi wa Vyama kuyumba na kudhoofisha Maendeleo ya Vyama hivyo.

Alisema kuuza mazao kwenye mifumo isiyo rasmi ni kumkosesha Mkulima haki anayostahiki kuipata. Hivyo alisitiza ni wajibu wa viongozi kuendelea kutoa elimu kwa wakulima wao juu ya umuhimu wa kuuza mazao yao kwa taratibu za kiushirika kwa kufuata mifumo iliyowekwa.

# STAKABADHI ZA GHALA KUPAISHA USHINDANI WA SOKO KWA MAZAO YA WAKULIMA



*Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara Mhe. Exaud Kigahe alipotembelea banda la Stakabadhi za Ghala wakati wa Siku ya Stakabadhi za Ghala katika Maadhimisho ya Wiki ya Ushirika Duniani yaliyofanyika Mjini Tabora.*

Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mhe. Exaud Kigahe, ametoa wito kwa kila Mdau anayehusika katika matumizi na usimamizi wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kutimiza wajibu wake katika nafasi yake ili kupata masoko ya mazao ya wakulima yenye ushindani.

Mhe. Kigahe ameyasema hayo Juni 28, 2023 wakati wa Siku ya Stakabadhi ya Ghala kwenye wiki ya Maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani iliyoanza Juni 26, 2023 na kilele cha Maadhimisho kufanyika Julai 01, 2023 katika Viwanja vya Nanenane Mjini Tabora.

Alisema matumizi ya Stakabadhi za Ghala yana umuhimu katika kukuza sekta ya biashara na masoko ya bidhaa nchini. Hivyo, wadau wanaohusika na Mfumo huu wakiwemo wakulima, watendaji katika Vyama vya Ushirika, wasimamizi wa maghala kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Stakabadhi za Ghala ili kukuza ushindani wa soko kwa kuwapa wakulima bei nzuri yenye tija.

"Kama mnavyofahamu, Mfumo wa Stakabadhi za Ghala unajumuisha wadau mbalimbali wakiwemo Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Waendesha Ghala, Mameneja Dhamana, Wakulima na Wazalishaji wa bidhaa nyingine, Taasisi za Fedha, Kampuni za Bima, Wakaguzi wa Ghala, Vyama vya Ushirika na Soko la Bidhaa Tanzania (TMX). Ufanisi katika kufikia malengo ya Mfumo unategemea utekelezaji wa wajibu wa kila mdau," alisema Mhe Kigahe.

## SACCOS LAZIMA KUJISAJILI ILI KUPATA LESENI - GAVANA



*Gavana wa Benki kuu ya Tanzania (BOT) Bw. Emmanuel Tutuba akizungumza na Viongozi wa TCDC, SACCOS, na Wadau wengine wa Ushirika wakati wa Uzinduzi wa Taarifa ya Utendaji wa Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS) uliofanyika Jijini Mwanza Septemba 22,2023*

Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania Bw. Emmanuel Tutuba alivitaka Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) kupata leseni kabla ya tarehe 30 Aprili, 2024 ili SACCOS hizo kuleta tija kwa wanaushirika na taifa kwa ujumla.

Gavana alitoa wito huo tarehe 22 Septemba, 2023 wakati wa hafla ya uzinduzi wa Taarifa ya Utendaji wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) kwa mwaka 2022 iliyofanyika Jijini Mwanza.

"Napenda kuwakumbusha kwamba muda wa mpito wa kupata leseni hizo uliotolewa na Benki Kuu unakaribia kuisha, muda huo utaisha mnamo tarehe 30 Aprili 2024. Hivyo, ni vema SACCOS hizo zikatumia muda huu uliobaki," alisema Gavana.

Aidha, Gavana alitoa wito kwa SACCOS zote Tanzania Bara kuendelea kuupa nguvu muungano wao ili uweze kuwahudumia vema wanachama.

# SACCOS ZAENDELEA KUPAISHA MAENDELEO NCHINI




*Gavana wa Benki ya Tanzania Mhe. Emmanuel Tutuba akizindua Taarifa ya Utendaji wa Vya ma vya Akiba na Mikopo (SACCOS) ya mwaka 2022 uliofanyika Jijini Mwanza Septemba 22, 2023.*

Naye Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Prof. Alfred Sife, akiongea kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika alisema kuwa Tume itaendelea kushirikiana na SACCOS ili kufikia malengo ya kukua kiuchumi.

Akiwasilisha Taarifa ya Utendaji wa SACCOS, Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Dkt. Benson Ndiege alisema kuwa SACCOS zinatakiwa kusajiliwa kwa mujibu wa sheria ya Vyama vya Ushirika kabla ya kuomba na kupewa leseni za kutoa Huduma Ndogo za fedha.

"Chama kikisajiliwa kinakuwa na sifa za kuomba na kupewa leseni ya huduma ndogo za Fedha kwa mujibu wa sheria ya huduma ndogo za fedha na Kanuni zake."

# VIONGOZI WA VYAMA WATAKIWA KUTEKELEZA VIPAUMBELE VYA USHIRIKA

Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson, amewataka Viongozi wa Vyama vya Ushirika Nchini kutekeleza vipaumbele saba vya kuzingatia katika uendeshaji wa Vyama ili kuleta mabadiliko katika Sekta ya Ushirika hapa nchini.



*Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania Dkt.Benson Ndiege akizungumza wakati akiwasilisha Taarifa ya Hali ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania Bara katika kikao cha Warajis Wasaidizi, Viongozi na Watendaji wa Vyama vya Upili kilichofanyika Jijini Dodoma Septemba 11,2023*

Mrajis ameyataja maeneo hayo saba Septemba 11, 2023 alipokuwa akiwasilisha Taarifa ya Hali ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania Bara katika kikao na Warajis Wasaidizi na Viongozi na Watendaji wa Vyama vya Upili kilichofanyika Jijini Dodoma.

"Tume na wadau wa Ushirika tumekubaliana kwamba Maeneo haya saba ndiyo yawe mwongozo na mwelekeo wa Maendeleo ya Ushirika," alisema Dkt Ndiege.



*Warajis Wasaidizi, Viongozi na watendaji wa Vyama vya Upili wakiwa kwenye kikao cha uwasilishaji wa Taarifa ya Hali ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania Bara kilichofanyika Jijini Dodoma Septemba 11, 2023.*

Akiyataja maeneo hayo saba kuwa ni: Uwekezaji katika mifumo ya kisasa ya kidigitali; uanzishaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika; kuhamasisha Mfumo wa Ushirika kujiendesha kibiashara; Usimamizi wa Vyama vya Ushirika; kuhamasisha Ushirika kwenye Sekta mbalimbali na makundi maalum; kushirikiana na wadau mbalimbali kutatua changamoto za Ushirika; na kuimarisha uwekezaji wa Mali za Ushirika katika uzalishaji.

"Lengo la kikao hiki ni kupata uhakika wa kila Mkoa kwenye maeneo haya, wao wamejipangaje ndipo tutauweka Ushirika mahali pake" ameongeza Mrajis.

Aidha, katika kikao hicho Dkt.Ndiege amewapongeza Watendaji mbalimbali wa Vyama vya Ushirika, wakiwemo Maneneja na Wenyeviti wa Vyama kwa kufanya Vizuri katika kuleta maendeleo na kuujenga Ushirika mpya.

"Watendaji mbalimbali wa Vyama vya Ushirika, wakiwemo Maneneja na Wenyeviti wa Vyama, hongereni sana, mnafanya vizuri, kazi mnayofanya ni nzuri na inaonekana," alisema Dkt. Ndiege.

## URA SACCOS YAZINDUA MATUMIZI YA MFUMO WA KIDIGITALI

Usalama wa Raia SACCOS imezindua Mfumo wa kidijitali wa huduma za kifedha uitwao (URA MOBILE MONEY) utakaotumiwa na Viongozi pamoja na Wanachama wa URA SACCOS. Uzinduzi umefanyika katika Chuo cha Taaluma ya Polisi jijini Dar es Salaam Septemba 30, 2023.




*Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhe. Jumanne Sagini, akizungumza wakati wa Uzinduzi wa Mfumo wa kidigitali wa Huduma za Kifedha (URA MOBILE MONEY) uliofanyika Jijini Dar es salaam.*

Akizungumza katika hafla fupi ya Uzinduzi wa Mfumo huo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhe. Jumanne Sagini, amelipongeza Jeshi la Polisi nchini kwa kutambua umuhimu wa kuwa na huduma za kifedha zinazotolewa na kupatikana kwa gharama nafuu kwa Watumishi wake na hivyo kuanzisha Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) miaka 17 iliyopita.

"Nafahamu kama ilivyoelezwa kwamba, tangu kuanzishwa kwa Ushirika huu tarehe 6 Septemba 2006, na kuutambua katika Kanuni za Kudumu za Utendaji za Jeshi la Polisi (P.G.O 212) fursa

mbalimbali zimetolewa kwa Watumishi kama vile uwekaji wa akiba na utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu ukilinganishwa na taasisi nyingine za kifedha," alisema Mhe. Sagini.

Pia alisema kuwa uwepo wa URA SACCOS kumechangia ustawi wa Watumishi kiuchumi, kurahisisha utendaji, kuongeza ufanisi katika kazi na kuongeza heshima kubwa kwa Watumishi wa Jeshi la Polisi kwa kuboresha maisha na kuwaepusha kujiingiza kwenye vitendo vya rushwa pindi wanapokabiliwa na mahitaji ya kifedha kwa ajili ya maendeleo yao.

"Kwa kufanya hivi mmeunga mkono kwa vitendo juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, ambaye kwa nyakati tofauti amesisitiza kuwekeza kwenye matumizi ya TEHAMA katika utekelezaji wa majukumu ya Umma," alisema Mhe. Sagini.

Pia Naibu Waziri Sagini alimpongeza Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Camillus Wambura, Bodi ya URA SACCOS na watendaji wa URA SACCOS kwa ubunifu, ueledi na umahiri wa kukivusha Chama kutoka kwenye mfumo wa analojia kwenda kwenye mfumo wa kidigitali kwa lengo la kuongeza uwazi na uwajibikaji.



*Wanachama na Viongozi wa Jeshi la Polisi (URA SACCOS) wakiwa katika hafla ya uzinduzi wa Mfumo wa Kidigitali wa Huduma za Kifedha iliyofanyika Jijjini Dar es salaam*

Aidha, URA SACCOS LTD ni miongoni mwa taasisi zenye kutoa mikopo yenye riba nafuu kuliko taasisi nyingine za kifedha lakini pia kutambua mafanikio muhimu yaliyopatikana katika Chama tokea kuanzishwa kwake mwezi Septemba 2006 ni kuongezeka kwa idadi kubwa ya Wanachama wanaofikia 45,142 Juni 30, 2023 ikilinganishwa na Wanachama 4,300 waliojiunga mwaka 2006 Chama kilipoanzishwa.

## ATAKAYESHIRIKI KUHUJUMU UBORA WA KOROSHO ZA NANYAMBA HATUTAMFUMBIA MACHO - MBUNGE CHIKOTA

Mbunge wa Jimbo la Nanyamba, Mhe. Abdallah Chikota, amewataka wakulima wa zao la Korosho katika jimbo hilo kuhakikisha wanazingatia ubora wa Korosho kabla ya kuzipeleka sokoni.



*Mbunge wa Jimbo la Nanyamba Mhe. Abdallah Chikota akizungumza na wananchi wa Jimbo lake katika kikao kazi kilichoandaliwa na Chama Kikuu cha MAMCU LTD kilichofanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya mji wa Nanyamba Septemba 27, 2023*

Mbunge Chikota amesema hayo Septemba 27, 2023 katika kikao kazi kilichofanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya mji wa Nanyamba kilichoandaliwa na Chama Kikuu Cha Ushirika wa wilaya za Masasi, Mtwara na Nanyumbu (MAMCU LIMITED) kwa kushirikiana na viongozi wa Vyama vya Msingi wa Halmashauri ya Mji wa Nanyamba.

Kikao hicho kilichokuwa na lengo la kutoa elimu juu ya kusimamia ubora wa zao la Korosho kabla ya kuingia sokoni, ambapo Mbunge Chikota alikuwa Mgeni Rasmi.

"Hatupo tayari kuona wananchi wanaipa lawama Serikali kutokana na Korosho za Nanyamba kukosa ubora.



*Wanachama na Viongozi wa Vyama vya Msingi vya Masasi, Mtwara na Nanyumbu (MAMCU LTD) wakiwa katika kikao kazi kilichofanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya mji wa Nanyamba Septemba 27,2023.*

"Mimi kama Mbunge nimekuja kuzungumza na ninyi viongozi wenzangu ambao ni watu muhimu sana katika kudhibiti ubora wa Korosho zetu kwasababu kama Korosho hazitokuwa bora basi tusitegemee bei yenye kueleweka na mimi kwa nafasi yangu sipo tayari kuona serikali ya CCM inaingia doa kwasababu ya Korosho ya Nanyamba haina ubora, atakayeshiriki kuhujumu ubora wa Korosho hatutamvumilia," alisema Mhe.Chikota

## MINADA SITA YA MBAAZI MAMCU YAINGIZA SHILINGI BILIONI 23.6

Chama Kikuu cha Ushirika cha Wilaya za Masasi, Mtwara na Nanyumbu (MAMCU LTD) kimeuza mbaazi tani 671 zenye thamani ya Shilingi Bilioni 1.3.



*Wakulima wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Wilaya ya Masasi, Mtwara na Nanyumbu wakiwa katika mnada wa sita wa zao la mbaazi ulifanyika katika Chama cha Msingi cha Chipuputa Wilayani Nanyumbu mkoani Mtwara.*

Chama Kikuu cha Ushirika cha Wilaya za Masasi, Mtwara na Nanyumbu (MAMCU LTD) kimefanya mnada kwenye Chama cha Msingi cha Chipuputa (AMCOS) kilichopo kijiji cha Chipuputa Wilayani Nanyumbu Mkoani Mtwara. Mnada huo ni wa sita na wa mwisho katika msimu wa mauzo kwa mwaka 2023/24.

Meneja wa MAMCU Tawi la Masasi, Costantine Leula alisema, kupitia mnada huo Wakulima wameuza tani 671 zenye thamani ya Sh bilioni 1.3 huku mnada wa kwanza mpaka wa sita Wakulima waliuza Mbaazi zenye thamani ya Shilingi bilioni 23.6.

Mkuu wa Wilaya ya Nanyumbu Mkoani Mtwara, Mariam Chaurembo amewapongeza wananchi wa Wilaya hiyo kwa kuendelea kulima mazao mengine mbadala wa Korosho ikiwemo Ufuta, Mbaazi na mazao mengine ya chakula.

Amewasisitiza kuwa, Wilaya hiyo ina ardhi ya kutosha na yenye rutuba hivyo mazao yote yanahitajika. Kwahiyo wakati wanaandaa mashamba msimu wa kilimo mwaka huu wazingatie mazao makuu matano ikiwemo Mbaazi, Korosho, Ufuta, Karanga, Choroko na mengine ili waweze kupata mapato ya uhakika.

"Niwapongeze sana wananchi kwa kuona umuhimu wa mazao mengine mbadala ya kulima, niwapongeze sana mmelima sana Ufuta mwaka huu, mmelima na Mbaazi na mengine ya chakula hongereni sana," alisema Chaurembo.

Alisema wanapoelekea kwenye msimu huo wa kilimo, serikali imeliingiza zao la choroko kwenye ushirika huo ambapo sasa inapambana kuona namna ambavyo zao la karanga litaingia kwenye ushirika.

## KACU IMENUNUA NA KUCHAKATA KILO MILIONI 4.6 ZA PAMBA

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Mhe. Christina Mndeme, amefurahi kusikia kuwa Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU) kinanunua na kuchakata Pamba ya wakukima wake ambapo zaidi ya kilo Milioni 4.6 imenunuliwa kutoka Ushetu, Msalala, Kahama na Kishapu.



*Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Mhe. Christina Mndeme akitembelea kiwanda cha Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU) Septemba 18, 2023 mkoani Shinyanga.*

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga ametembelea kiwanda cha KACU tarehe 18 Septemba, 2023 na kujionea jinsi Ushirika unavyoongeza thamani ya mazao yake ambapo katika ziara yake aliambatana na Viongozi mbalimbali wa Mkoa, Wilaya ya Kahama, Viongozi wa CCM, Mhe. Mbunge wa jimbo la Ushetu, Benki ya CRDB na wadau mbalimbali wa Ushirika.

Katika kukagua shughuli zinazofanywa na kiwanda hicho amepongeza Ushirika kwa kusaidia Serikali kutoa ajira kwa wanawake na vijana zaidi ya wafanyakazi 174, na kiwanda kutoa fursa kwa mamalishe ambao wanauza chakula maeneo ya jirani na kiwanda.



*Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Mhe. Christina Mndeme akitembelea kiwanda cha Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU) Septemba 18, 2023 mkoani Shinyanga.*

"KACU inalenga kumsaidia mkulima na mwanaushirika, kwa jinsi ushirika huu unavyosimamiwa vizuri, Serikali itaendelea kuwa na imani kubwa na Ushirika kuwa ndio nguzo ya kumkomboa Mkulima na mwananchi wa uchumi wa chini," alisema Mkuu wa Mkoa.

# TAMCU LIMITED WAUZA TANI 4,789 ZA UFUTA WENYE THAMANI YA SHILINGI BILIONI 17.6



*Wakulima wa zao la Ufuta wa Chama Kikuu cha Ushirika Wilaya ya Tunduru Mkoani Ruvuma (TAMCU LTD) wakishuhudia mnada wa zao hilo uliofanyika Julai 27, 2023 katika Ofisi za Chama hicho*

Chama Kikuu cha Ushirika Wilaya ya Tunduru (TAMCU LTD) kilichopo mkoani Ruvuma Julai 27, 2023 kimefanya mnada wake wa Saba katika ofisi za chama hicho ambao ni mnada wake wa mwisho kwa msimu wa kilimo wa zao hilo. Katika mnada huo mnunuzi mmoja alijitokeza kuomba zabuni ya kununua ufuta wote tani 4,789 kwa Shilingi Bilioni 17.6.

Meneja Mkuu wa TAMCU LTD Imani Kalembo amewaeleza wakulima wa Wilaya ya Tunduru kuwa mnada huo ni wa mwisho na sasa maandalizi yapo katika kilimo cha zao la mbaazi. Alisema dhamira ya Chama hicho ni pamoja na kuuza Mbaazi kwa njia ya Stakabadhi ya Mazao Ghalani na walitaka wakulima kuendelea kutumia mfumo huo kwani unawapa uhakika wa soko na bei nzuri ya Mazao yao.

"Sasa ndugu zangu tuwekeze nguvu zetu kwenye kilimo cha mbaazi na korosho ambacho kinatarajia kuanza hivi Karibuni,”. alisema Kalembo.

## BEI YA KAKAO YAPAA YAFIKIA SHILINGI 8,825 KWA KILO MOJA

Mnada wa 11 wa Kakao umefanyika Septemba 11, 2023 katika Ghala kuu la KYECU LTD Wilayani Kyela katika Mkoa wa Mbeya na wakulima kuuza Kakao zote kwa bei ya Shilingi 8,825/= kwa kilo moja.




*Wakulima wa kakao wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Kyela (KYECU LTD) wakiwa katika mnada wa 11 uliofanyika katika ofisi za chama hicho Septemba 11, 2023.*

Kampuni ya Ununuzi ya Mohamed Interprises (T) LTD ndiyo iliyonunua Kakao zote zenye jumla ya kilo 251,710 katika mnada huo.

Wanunuzi wengine walioshiriki katika mnada huo ni 4C PROTRADE kwa bei ya shilingi 8,470/= na Kampuni ya E.T.G kwa bei ya shilingi 8,655/=.

## TANI 10.9 ZA MBAAZI ZAKUSANYWA NA KUUZWA KATIKA MINADA MITANO MAMCU

Chama Kikuu cha Ushirika cha MAMCU LTD Septemba 8, 2023 kimefanya mnada wa tano wa Wakulima wa zao la Mbaazi kijiji cha Chikundi Wilaya ya Masasi Mkoani Mtwara wamekubali kuuza Mbaazi kwa bei ya juu ya Shilingi 2,130 na bei ya chini Shilingi 2,120 kwa kilo moja.



*Wakulima wa zao la Mbaazi wa Chama Kikuu cha Ushirika cha MAMCU LTD wakiwa katika mnada wa tano wa zao hilo uliofanyika Septemba 8, 2023.*

Kaimu Meneja wa Chama cha Ushirika MAMCU Tawi la Masasi, Constatina Frances, alisema kuwa mnada wa 5 umekusanya kilo 925,667 na kufanya jumla ya Tani 10.9 katika minada mitano; amewaomba wakulima wa zao la Mbaazi kuendelea kukusanya mbaazi zenye ubora ili kuwahamasisha wanunuzi kuongeza bei ya zao hilo.

Constatina ameishukuru Serikali ya Awamu ya sita kwa kuendelea kuimarisha bei na kumfanya mkulima ananufaika kutoka kwenye kuuza mbaazi kwa bei ya Shilingi 200 hadi kufikia bei ya Shilingi 2,000 na kuendelea.

## MWAYA AMCOS YACHANGIA BATI ZA SHILINGI 1,080,000 KUSAIDIA UJENZI WA OFISI ZA VIJIJI

Chama cha Ushirika cha Msingi Mwaya AMCOS Kimechangia mabati yenye gharama ya shilingi 1,080,000 kusaidia ujenzi wa ofisi za Vijiji vya Ndola na Lugombo katika Kata ya Mwaya, Wilayani Kyela Mkoani Mbeya.



*Wanachama wa Chama cha Ushirika cha Msingi Mwaya wakichangia mchango wa mabati kusaidia ujenzi wa Ofisi Vijiji vya Ndola na Lugombo katika kata ya Mwaya Wilaya ya Kyela, Mkoani wa Mbeya Septemba 06,2023.*

Walitoa mchango huo Septemba 06, 2023 ikiwa ni kutimiza Msingi namba 7 wa Ushirika wa kuijali jamii.

## WAKULIMA WA MBAAZI MANYARA WAFURAHIA KUUZA MBAAZI KWA MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA KUPITIA USHIRIKA

Wakulima wa Mbaazi mkoani Manyara tarehe 5 Septemba, 2023 wamefanya mnada wa kwanza uliofanyika Wilayani Kiteto na wameuza Mbaazi kwa bei ya shilingi 2,261 kwa kilo moja kwa Kampuni ya ununuzi ya H.S IMPEX.



*Wakulima wa Mbaazi wa Chama Kikuu cha Ushirika ACU LTD wakiwa katika mnada kwanza wa zao hilo uliofanyika katika Ghala kuu la Chama Kikuu cha Ushirika ACU LTD Septemba 05, 2023*

Wakulima wamekubali kuuza mbaazi zote zenye jumla ya kilo 250,000 katika Ghala la Chama Kikuu cha Ushirika ACU LTD.

Wanunuzi wengine walioshiriki katika mnada huo ni SEDACO (2,105/), YURI Investment (2,050/), Export Trading (2,168/), SM Holding (2,261/) na AFRISSAN (2,050/).



*Wakulima wa Mbaazi wa Wilayani Tunduru wakiwa katika mnada wa kwanza wa zao hilo uliofanyika, Agosti 12, 2023*

Mnada huo umefanyika Wilayani Tunduru tarehe 12/08/2023 na Kampuni tatu zimeshinda katika mnada huo.

## *MKATABA WA HUDUMA KWA MTEJA WA TCDC*

Tume ya Maendeleo ya Ushirika ikiwa ni Taasisi inayojitegemea ina jukumu la kuhudumia Vyama vya Ushirika na wadau mbalimbali wa sekta ya Ushirika. Mkataba huu wa Huduma kwa Mteja utawawezesha wateja kuelewa ***Huduma, Viwango vya muda*** na ***Ubora wa Huduma*** zinazotolewa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania.

Mkataba huu unaainisha viwango vya huduma ambavyo Wateja wetu wana haki ya kupata na pia kuweka utaratibu wa ufuatiliaji na utatuzi wa changamoto pale zinapojitokeza. Mkataba umeandaliwa kwa kuwashirikisha wateja wadau pamoja na watumishi. Mkataba huu utasaidia Taasisi kuweza kuboresha utoaji wa huduma kwa wateja wake na pia kupata mrejesho wa huduma zitolewazo. Hivyo tunaamini Mkataba huu utakuwa chachu ya kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

Tunatarajia Mkataba wa ***Huduma kwa Mteja*** utaweza kujenga maelewano mazuri ya kikazi kati ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania na wateja wetu, na kusaidia kufikia lengo la kutoa na kuboresha huduma zetu kwa ufanisi.

***Dira ya TCDC***

Kuwa Taasisi mahiri ya Uthibiti kwa Maendeleo ya Ushirika Tanzania.

***Dhima ya TCDC***

Kutoa huduma za udhibiti na uhamasishaji zenye ufanisi na ubora ili kuwa na Ushirika wenye nguvu, ubunifu na endelevu kiuchumi.

***MAADILI YETU***

Ili kutoa huduma zetu kwa ufanisi tutaongozwa na Maadili muhimu tuliyojiwekea kama ifuatavyo;

***Uadilifu***

Tutafuata viwango vya juu vya mwenendo katika kila tunachokifanya. Tutatimiza ahadi zote kwa maslahi ya Taasisi na Taifa kwa ujumla.

***Uwajibikaji***

Tutatekeleza majukumu na kuwajibika kwa matokeo

***Ushirikiano***

Tutafanya kazi kwa pamoja ili kutekeleza malengo kwa kubadilishana stadi, ujuzi na uzoefu.

***Weledi***

Tutatoa huduma zetu kulingana na ujuzi wa kiufundi na stadi husika.

***Utendaji unaozingatia Matokeo***

Tutafanya kazi kwa mahitaji ya wateja wetu na matokeo yaliyotarajiwa.

***Uwazi***

Tutafanya kazi kwa uwazi, tutawasiliana kwa lugha inayoeleweka na kuwapatia wateja wetu taarifa zote kuhusu huduma zetu, gharama zake na mafanikio ya Taasisi kila mwaka.

***Kuthamini wateja***

Tutajitoa kwa dhati Kuwasaidia wateja wetu, kutimiza malengo yao kwa kuelewa shughuli wanazozifanya na kuwapa kile wanachokithamini.

***Ubunifu***

Tutazingatia utamaduni wa Tume unaothamini uasili wa kujiendesha kibiashara, uvumbuzi na ubunifu katika kuiwezesha sekta ya Ushirika.

***MADHUMUNI YA MKATABA***

Madhumuni ya Mkataba wa Huduma kwa Mteja ni kuwafahamisha wateja wa TCDC juu ya viwango na ubora wa Huduma zitolewazo na Tume ya Maendeleo ya Ushirika. Aidha, Mkataba huu unabainisha utaratibu ambao mteja ataufuata katika kuwasiliana, kupata huduma na kutoa malalamiko, pongezi, maoni au mapendekezo juu ya ubora wa huduma zinazotolewa na TCDC.

***WATEJA WETU***

Tume ya Maendeleo ya Ushirika inatoa huduma kwa wateja wa Taasisi kama ifuatavyo: -

***Wateja wetu ni:***

1. Wanachama wa Vyama vya Ushirika.
2. Vyama vya Ushirika;
3. Wizara, Idara zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa, Wakala za Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa, na Taasisi.
4. Watoa huduma kwenye vyama vya Ushirika.
5. Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MOCU) na Taasisi zingine za Elimu.
6. Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa.
7. Makampuni.
8. Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO).
9. Wananchi.

10. Watafiti.

11. Watoa huduma kwa Taasisi;

12. Wanasiasa na

13. Vyombo vya Habari.

14. Taasisi za Kifedha.

***HUDUMA ZETU***

Tume ya Maendeleo ya Ushirika inatoa huduma kwa wateja wake mbalimbali kama ifuatavyo;

1. Usajili wa Vyama vya Ushirika
2. Leseni za uendeshaji wa Vyama vya Ushirika
3. Vibali mbalimbali
4. Taarifa mbalimbali
5. Tatuzi za Migogoro,
6. Miongozo mbalimbali
7. Ushauri wa kitaalamu
8. Elimu na Mafunzo
9. Idhini mbalimbali
10. Huduma nyinginezo

***Usajili wa Vyama vya Ushirika***

1. Tutatoa usajili wa Chama cha Ushirika ndani ya siku 30 baada ya kukidhi vigezo
2. Tutatoa usajili wa rehani ya chama cha Ushirika ndani ya siku 30 baada ya kuidhinishiwa Hati ya ukomo wa madeni
3. Tutatoa usajili wa Masharti, Kanuni na Miongozo mbalimbali ya Chama cha Ushirika ndani ya siku 21 baada ya kupokea maombi
4. Tutatoa usajili wa Watoa Huduma kwenye Vyama vya Ushirika mwezi Juni kila mwaka
5. Kurejesha Usajili wa chama cha Ushirika kilichofutwa ndani ya siku 30 baada ya kukidhi vigezo vya kushinda rufaa Na. Leseni za uendeshaji wa Vyama vya Ushirika
6. Tutatoa leseni kwa chama cha Ushirika wa kifedha (SACCOS) ndani ya siku 60 baada ya maombi ya leseni

***Vibali mbalimbali***

1. Tutatoa vibali kwa watoa huduma mbalimbali katika Vyama vya Ushirika ndani ya siku tano (5) baada ya usaili
2. Tutatoa vibali vya ajira kwenye vyama vya Ushirika ya siku 14 baada ya kupokea maombi

***Elimu na Mafunzo***

1. Tutatoa Elimu kwa wanachama wa Vyama vya Ushirika kuhusu mambo ya Ushirika siku saba (7) baada ya maombi kutolewa

2. Tutatoa Elimu ya Ushirika na manufaa yake kwa jamii ndani ya siku saba (7) baada ya kuona uhitaji wa ushirika

3. Tutatoa Mafunzo kwa Viongozi na Watendaji wa Vyama vya Ushirika ndani ya siku 14 baada ya kupokea maombi

4. Tutatoa Mafunzo ya mfumo wa MUVU kwa Viongozi na Watendaji wa Vyama vya Ushirika kila mwaka

5. Tutatoa Mafunzo ya uzingatiaji wa sheria katika uendeshaji wa shughuli mbalimbali za Vyama vya Ushirika kila robo mwaka

***Ushauri wa kitaalamu***

1. Tutatoa ushauri wa maeneo yanayotakiwa kufanyiwa marekebisho ya Kanuni na Miongozo inayohusiana na Vyama vya Ushirika ndani ya siku 5 baada ya kupokea maombi

2. Tutatoa ushauri wa kisheria ndani ya siku tano (5) baada ya kupokea maombi na Huduma nyinginezo

I. Tutakiri kupokea barua ndani ya siku tatu (3)

II. Tutajibu hoja za barua zilizopokelewa ndani ya siku saba (7) za kazi

III. Tutapokea simu ndani ya miito mitatu (3)

IV. Tutaboresha tovuti ya Tume kila mwaka

***Itaendelea Toleo lijalo……………***

# HABARI KATIKA PICHA






TUME YA MAENDELEO YA
USHIRIKA TANZANIA TCDC


Maelezo
2019
AGRF
AFRICA FOOD
SYSTEMS FORUM
2023




JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
UME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA (TCDC)
A TAARIFA YA UTENDAJI WA VYAMA VYA USHIRIKA WA
KIBA NA MIKOPO (SACCOS) KWA MWAKA 2022
CHING OF SACCOS ANNUAL PERFORMANCE REPORT, 2022








CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA CHA WAKULIMA
WA TUMBAKU CHUNYA (CHUTCU LTD)
MAADHIMISHO YA NANENANE 2023
KAULI MBIU:
VIJANA NA WANAWAKE













*Limetolewa na:*
*Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC)*
*Mtaa wa Kuu, S.L.P 201, DODOMA.*
*Simu: +255 26 2322456, Telefax: +255 26 23 21973*
***B. pepe:** ushirika@ushirika.go.tz* ***Tovuti:** www.ushirika.go.tz*